

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 25 Vol. 89 dated 20th June, 2008
Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 83 la tarehe 20/6/2008

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu vya 6 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KUEGESHA MAGARI) ZA HALMASHAURI YA
MANISPAA YA MOROGORO, 2008.

- | | |
|--|-----------|
| 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kuegesha Magari) za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, 2008 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. | Jina |
| 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika kwenye eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. | Matumizi |
| 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakavyoelezwa vinginevyo:
"Afisa mwidhinishwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia Sheria Ndogo hizi;
"Halmashauri" ina maana ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro;
"Kituo cha basi" maana yake ni kituo kilichoidhinishwa na Halmashauri ambapo mabasi yanayotoa huduma ya usafiri kwa umma, hupakia na kushusha abiria;
"Maagesho yaliyotengwa" maana yake ni sehemu yaliyotengwa maalum ya kuegesha gari; | Ufafanuzi |

